

Katiba ya Jumuiya ya Zanzibar Diaspora- Skandinavia

Kutokana na kuwepo kwa idadi kubwa ya Wazanzibari katika nchi za Skandinavia, na kwa nia ya kuwasaidia ndugu zetu walioko Zanzibar, pamoja na kuunga mkono jitihada za Ofisi ya Raisi wa Zanzibar inayoshughulika na masuala ya diaspora, imeonekana ipo haja ya kuunda Jumuiya itakayo wakumbusha Wazanzibari wajibu wao wa kuisaidia nchi yao- Zanzibar, sambamba na kuunganisha umoja na mshikamano wao popote walipo.

1. Jina

Jumuiya hii inayoanzishwa kwa mujibu wa Katiba itaitwa “Zanzibar Diaspora-Skandinavia.”

2. Hadhi

Jumuiya itakuwa ni chombo huru kinachojitegemea kwa jina lake mwenyewe kuweza kumiliki mali pamoja kuwa na uwezo kushitaki ama kushitakiwa.

3. Lugha

Katika utendaji wa shughuli zake za kawaida za kila siku jumuiya itatumia lugha ya Kiswhili, Kingereza au Kidenish kwa mujibu wa mahitaji.

4. Ofisi na anuani

Ofisi ya Jumuiya itakuwa katika jiji la Copemhagen-Denmark. Anuwani yake itakuwa ni kama ifatavyo-;

C/O Hashil Seif Hashil
Gustav Bangs Gade 11st, th
Denmark.
Simu: 0045-20726491
Email: thinktank1917@gmail.com

5. Madhumuni

Jumuiya ya Zanzibar Diaspora-Skandinavia itakuwa na madhumuni yafuatyo:

- Kuleta mapenzi, umoja na maendeleo mingoni mwa Wazanzibari wote walioko ughaibuni na walioko nyumbani
- Kuendeleza heshima na kulinda mila, utamaduni na maadili ya Kizanzibari
- Kuwahamasisha Wazanzibari kuipenda na kuithamini nchi yao
- Kulinda na kutetea haki za binaadamu
- Kushirikiana na wenyeji wetu Denmark na nchi nyingine za Skandinavia ili kuendeleza amani, haki na usawa katika jamii hizi
- Kusaidia kutatua na kukabili matatizo yanayoikumba jamii ya Zanzibar

- Kupanga au kusaidia shughuli yoyote yenye lengo la kuisaidia Zanzibar
- Jumuiya hii itakuwa huru, isiyofungamana na siasa au dini ya upande wowote

6. Uanachama

(a) Kila Mzanzibari mwenye umri usiopungua miaka 18, na ambae atakuwa tayari kutii na kuifata katiba hii anaweza kuwa mwanachama wa Zanzibar Diaspora-Skandinavia

(b) Maombi ya uanachama yatafanywa kwa kujaza fomu maalumu itakayowekwa kwa ajili hiyo

(c) Kulingana na masharti yaliyowekwa na katiba hii, kila mwanachama anakuwa na haki zifuatazo:

- kushiriki na kutoa mapendekezo katika shughuli zote za jumuiya.
- Kuchagua ama kuchaguliwa kushika nafasi yoyote ile ya uongozi.

(d) Kila mwanachama atakuwa na wajibu kama ifuatavyo:

(i) Kulipa ada maalumu ya kujiunga na jumuiya. Ada hii haitarudishwa kwa mwanachama iwapo ataamua kuacha uanachama au kwa hali yoyote ile.

(ii)Kulipa ada ya kila mwezi/mwaka kama itakavyowekwa na kukubaliwa na kamati kuu

(e) Mwanachama atapoteza sifa za kuwa mwanachama iwapo moja kati ya haya litatokea:

- Kuacha kwa hiyari
- Kuachishwa uanachama na kamati kuu
- Kufariki

7. Vyombo vya utawala

(a) Mkutano Mkuu. Huu utafanywa kila mwaka mara moja, na wanachama watajulishwa angalau mwezi mmoja kabla ya tarehe ya mkutano

(b) Kamati Kuu. Hii haitozidi watu watano wakiwemo mwenyekiti, katibu na mshika fedha.

(c) Mkutano wa dharura. Utaitishwa kwa mujibu wa haja na iwapo 2/3 ya wanachama watakubali kuitishwa kwa mkutano huo.

5. Viongozi wa Jumuiya

Katika utekelezaji wa shughuli za jumuiya, Zanzibar Diaspora-Skandinavia itakuwa chini ya usimamizi wa watu wafuatao:

- Mwenyekiti
- Msaidizi Mwenyekiti
- Katibu mkuu
- Mshika fedha

* Kutakuwa na mchunguzi wa fedha ambaye hatakuwa mjumbe wa kamati kuu.